

# MNR yafukuzwa mijini

U.S. LISBON, Ureno  
P. Z 12/12  
67

MAJESHI ya wananchi wa Msumbiji yameirejesha mikononi mwa serikali miji karibu yote ambayo ilikuwa imekaliwa na magaidi ~~mwa~~ MNR wanaoungwa mkono na utawala wa Makaburu wa Afrika Kusini, Rais Joaquim Chissano alisema katika mahojiano yaliyochapishwa jana.

"Hali ya kijeshi nchini imebadilika katika kipindi cha miezi 18 iliyopita na tumewafye ka magaidi katika karibu miji yote" alisema Ndugu Chissano katika mahojiano na televisheni ya Ureno ambayo nakala yake ilipatikana hapa.

"Vile vile tuliendelea na mapinduzi

yetu katika kilimo ingawa jitihada zetu ziliendelea kuathiriwa na hujuma za magaidi na ukame unaoikabili nchi yetu" alisema.

Hata hivyo, magaidi wa MNR wamekanusha kuwa walikuwa ~~wametimuliwa~~ katika miji yote ambayo walikuwa wakiishikilia.

"Tumepoteza miji kadhaa muhimu kijeshi lakini bado tunaimiliki mingine kadhaa na eneo karibu lote la vijijini kaskazini mwa nchi" taarifa ya magaidi hao ilidai.

Vile vile Rais Chissano alitoa mwito kwa nchi zilizoendelea zisiwasaidie magaidi kwa vile alisema mauaji ya kinyama yanayoendeshwa na magaidi hao dhidi ya raia wasio na hatia hayamfaidii mtu ye yote.